# Jibu la UVIKO-19 Barani Afrika: Pamoja kwa Taarifa za Kuaminika

Maelezo haya ni kwa niaba ya mradi wa Jibu la UVIKO-19 Barani Afrika: Pamoja kwa Taarifa za Kuaminika. Mradi huu umefadhiliwa na Umoja wa nchi za Ulaya

# Tanzania: Maelezo kuhusu kushambuliwa kwa waandishi wa habari Machi 2020–Julai 2021

## Muktasari

Global Expression Report 2021 alama:

**38/100**

**5**

Wahabari walionasawa na kuzuiliwa

**1**

Sheria zilizotekelezwa

## Taarifa hii kwa Muktasari

Waandishi – habari wanatoa mchango mkubwa kuhakikisha kuna uhuru wa kuongea na jinsi ya kupata taarifa, uhuru ambao unalindwa kwenye sheria za haki za binadamu ulimwenguni na katika katiba ya Tanzania. Uhuru huo wa vyombo vya habari unakuwa na umuhimu zaidi haswa wakati kunapotokea janga la ugonjwa kama UVIKO-19.

Hata hivyo, mabadiliko ya sheria yaliyofanyika nchini Tanzania mnamo mwaka wa kwanza wa kutangazwa kuwepo kwa UVIKO-19, haswa chini ya utawala wa Rais marehemu John Magufuli — ulikiuka uhuru wa wana — habari, na kuzuia kabisa uhuru wa vyombo vya habari, kama maelezo yafuatayo yanavyoonyesha.

Wakati tandavu ya UVIKO-19 ilipoingia Tanzania mnamo mwezi Machi 2020, Rais Magufuli alikataa uwepo wake na kupuuza athari zake na hata serikali ikasimamisha utoaji wa taarifa kwa wananchi kuhusu maambukizi na vifo mnamo tarehe 29 Aprili 2020. Baada ya wiki sita, Magufuli alitangaza kwamba wananchi walifanya maombi na kuangamiza kabisa virusi vya Corona nchini Tanzania, jambo ambalo lilizuia uhuru wa vyombo vya habari: Wana- habari wataandikaje taarifa kuhusu janga hili wakati kwenye mtazamo wa Rais, halikuwepo?

> Gonjwa la Corona limeangamizwa tunashukuru Mungu

Hayati Rais John Magufuli, June 2020

Mnamo tarehe 22 Mei 2020, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alitoa maagizo kuzuia upatikanaji na utoaji wa habari kuhusu UVIKO-19. Kuanzia hapo, ni Waziri wa Afya pekee aliyeruhusiwa kutoa taarifa kuhusu maambukizi ya Corona — na, ikibidi Waziri Mkuu mwenyewe. Hata kufikia mwisho wa mwezi Februari 2021, Waziri wa Afya Dorothy Gwajima alionya waandishi-habari kuhusu kutoa takwimu za Corona ambazo sio rasmi.

Sera hiyo ya serikali ya Tanzania ya kukataa uwepo wa janga la Corona mnamo mwaka wa kwanza, ilikuwa na athari kubwa kwa waandishi-habari ambao hawangeweza kuripoti kikamilifu juu ya janga hili kutokana na kuogopa kutiwa mbaroni — jambo ambalo lilikera sana jamii ya kimataifa, kuanzia Shirika la Afya Ulimwenguni(WHO) na Waandishi wasio na Mipaka(RWB).

---

Tunahimiza serikali ya Tanzania kufuata mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hii ili kuhakikisha uhuru wa wana-habari na usalama wao unadhaminiwa — haswa wakati huu wa UVIKO-19.




Waziri wa Afya Dorothy Gwajima, ambaye aliwaonya wana-habari dhidi ya kutoa taarifa ambazo sio rasmi mnamo Februari 2020 (Picha: Kwa niaba ya Shirika la habari la Nation)

## Majibu kuhusu taarifa za “uongo” na za “kupotosha”

Kuwalinda waandishi-habari na watetezi wa haki za binadamu, na kukomesha kutotii sheria kwa mashambulio dhidi yao, ni suala linalopewa kipaumbele duniani ili kulinda uhuru wa kujieleza. Vitisho,mashambulizi na kuzuia na kutiwa ndani kiholela -— na inapovuka mipaka,kupotezwa au kuuwawa kwa wana-habari na watetezi wa haki za binadamu — kunachangia pakubwa sio tu uhuru wa mtu kujieleza lakini pia unakiuka haki ya kuishi, maadili ya kimwili, na wakati mwengine, haki ya kiafya.

Kulingana na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu, uhuru wa kujieleza na kutoa taarifa hauwezi ukakandamizwa kwa sababu taarifa husika sio za kweli, hazina makusudio au zina kera.Na kama alivyosema Katibu wa mkutano mkuu wa umoja wa mataifa mwanzoni mwa kuzuka kwa UVIKO-19, kwamba “kuchukulia taarifa zisizo za kweli kuwa kosa la jinai, kutaweka uhasama kwenye taarifa za taasisi za serikali, kuchelewesha kupata kwa taarifa za kuaminika na kuwepo kwa kuzuia uhuru wa kujieleza.”

## Mhariri akamatwa kwa kuweka wazi athari za UVIKO-19 kwenye mitandao ya kijamii

Mnamo tarehe 6 Aprili 2020, Afrikana Mlay, Mhariri wa Kiswahili wa gazeti la *Kasheshe,* alitiwa nguvuni katika Mkoa wa Kilimanjaro kwa kudaiwa kueneza "taarifa zisizo za kweli" kwenye mtandao wa kijamii.Kwenye taarifa yake, Mlay alisema kwamba Tanzania inaficha ukweli kuhusu maambukizi ya UVIKO-19. Polisi walisema kwamba Mlay atashtakiwa mahakamani kwa kusambaza habari, ambazo polisi walidai, zilihatarisha usalama wa taifa na kuzua hofu. Hatua hii ilifuatia onyo la Waziri Mkuu wiki chache awali:

> Namuonya mtu yoyote dhidi ya kusambaza habari zisizo na msingi kupitia simu za mkononi na mitandao ya kijamii, ambazo zitazua hofu kwa wananchi, lazima watu kama hao washikwe na kuchukuliwa hatua

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, 21 Machi 2020

Wakati tukitayarisha taarifa hii mnamo mwezi Oktoba 2021, hatukuwa na taarifa zozote kwa umma kuhusu kesi ya Mlay.

---

## Mwanablogi atiwa ndani kwa matumizi "yasiyo sahihi ya mitandao ya kijamii"

Wiki hiyo hiyo aliyonaswa Mlay, mwanablogi Awadhi Lugoya alishutumiwa kwa kosa la "matumizi yasiyo sahihi ya mitandao ya kijamii" na alitiwa mbaroni kwa madai ya kufungua mtandao wa Facebook (Coronavirus Tanzania) kusambaza habari, ambazo kulingana na Kamanda wa polisi Mkoa wa Morogoro, "ulipotosha" kuhusu hali halisi ya Corona. Kosa la Lugoya anaweza kutozwa faini ya shilingi milioni 5 za Tanzania ( sawa na Dola 160 za Kimarekani) au miezi 12 jela chini ya Kanuni ya mwaka 2018 kuhusu Kanuni za Udhibiti Mawasiliano ya Posta na Kielektroniki.

Hakuna maelezo yoyote kwa umma kuhusu kesi ya Lugoya wakati tukitayarisha taarifa hii mnamo mwezi Oktoba 2021.

---

## Waandishi wa *Mwananchi* washtakiwa kwa kutoa taarifa kuhusu wanaougua UVIKO-19

Mnamo tarehe 30 Aprili 2020, waandishi wawili wa gazeti la *Mwananchi*, Haidary Hakam na Alona Tarimo, walitiwa mbaroni na kushtakiwa kwa kueneza taarifa zisizo za kweli kuhusu UVIKO-19 kwenye mtandao wa WhatsApp. Walishtakiwa chini ya Sheria za uhalifu wa kimtandao za mwaka 2015.Afisa Mkuu mwandamizi (SACP) wa polisi wa Kinondoni, Edward Bukombe, alitumia fursa hiyo kuwakumbusha watanzania kuacha kusambaza taarifa kwenye mitandao ya kijamii ambazo hazijathibitishwa na serikali au taasisi zake.

---

## Gazeti moja lafungiwa na kutozwa faini kwa kuchapisha picha ya Rais Magufuli kwa kutozingatia sheria za kuweka umbali wa mtu na mtu

Mnamo tarehe 21 Machi 2020, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa aliagiza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuchunguza na kuwanasa watu wanaotoa "habari za uongo" kuhusu UVIKO-19.

Wiki kadhaa baadae ( Aprili 17), TCRA ilifutilia mbali leseni ya gazeti la *Mwananchi* kwa miezi sita na kutozwa faini ya shilingi milioni 5 (Sawa na Dola 2,155 za kimarekani) kwa madai ya kukiuka sheria ya Mawasiliano ya Posta na njia za kielektroniki (Kwenye mtandao) ya mwaka 2018.

Hii ilitokea muda mfupi tu baada ya gazeti la *Mwananchi* kuchapisha picha ya Rais Magufuli akitangamana na watu wakati akinunua vitu madukani, kinyume na maagizo ya serikali ya kujikinga na virusi vya Corona na kuweka umbali unaostahili kati ya mtu na mtu. Picha hiyo ilizua mjadala mkali mitandaoni kuhusu juhudi za Tanzania katika kupambana na janga hilo. Serikali ilidai kwamba picha hiyo ilipigwa kabla ya kuingia kwa Corona huku gazeti la *Mwananchi* likilazimika kuomba msamaha na kuiondoa picha hiyo kwenye mtandao wao.

---

## Leseni ya Kwanza TV yafutwa kwa kutumia taarifa ya tahadhari kutoka ubalozi wa Marekani

Mnamo tarehe 10 Julai 2020, leseni ya kituo cha televisheni ya mtandao Kwanza TV ilifutwa kwa muda wa miezi 11 kwa kutumia taarifa ya tahadhari kutoka ubalozi wa Marekani kwenye mtandao wa Instagram. Taarifa hiyo ilionya kwamba visa vya maambukizi nchini Tanzania vinazidi kuongezeka.

Naibu Mwenyekiti wa kamati ya maelezo (kwenye mtandao) kwenye Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Joseph Mapunda, aliwaambia waandishi wa habari kwamba kituo cha Kwanza TV kimepeperusha hewani taarifa ambayo haikuwa sahihi, taarifa ambayo ilikusudiwa kuzua hofu na kuharibu uchumi wa nchi na kwamba taarifa hiyo ilikwenda kinyume cha sheria ya Mawasiliano ya Posta na njia za kielektroniki (Kwenye mtandao) ya mwaka 2018.

> "Haki yetu ya kusikizwa haikuzingatiwa kwani tulipewa chini ya muda wa saa 24 kujibu samansi ... tungependa kusisitiza kuwa Kwanza TV haiukuvunja sheria yoyote"

Taarifa ya kituo cha Kwanza Online TV

## Kubana taarifa za waandishi, kuzuia kupatikana kwa habari

### Vyombo vya habari vyazuiwa na kulazimishwa kuomba msamaha kwa kumtaja Rais Magufuli kwamba ni "mkaidi"

Tarehe 26 mwezi Aprili 2020, kampuni za Star Media, Multichoice Tanzania na Azam kitengo cha digitali, zilitozwa faini ya shilingi milioni 5 (sawa na dola 2, 200 za Kimarekani) kwa madai ya kukiuka mawasiliano ya UVIKO-19. Vituo hivyo vilipeperusha taarifa kutoka kituo cha Citizen Tv cha Kenya ambacho kilimtaja Rais Magufuli kuwa "mkaidi" kwa kukataa kufunga nchi kutokana na Corona kama ilivyokuwa imefanya Kenya.Vituo hivi vilitakiwa kutangaza msamaha kwa Rais Magufuli kwa siku saba mfululizo.Kituo cha Citizen TV na redio pia kilitakiwa kutangaza msamaha huo.

### "Jaribio la kiholela la kuzima sauti zinazokosoa"

Mnamo tarehe 11 mwezi Agosti 2020, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) iliweka sheria mpya iliyotaka vyombo vya habari kupata idhini ya serikali kabla ya kutangaza habari kutoka nje.Wanaharakati wa kupigania uhuru wa vyombo vya habari na viongozi wa upinzani, walipinga sheria hiyo mpya, ambayo walisema ni kujaribu kuzuia watanzania kupata taarifa muhimu kuhusu UVIKO-19.

> Hii ni jaribio la kiholela kujaribu kuzima sauti zenye kukosoa na uhuru wa kupata habari kabla ya uchaguzi nchini Tanzani … hatua hii ya kuthibiti vyombo vya habari ni vigumu kukabiliana nayo.
>
> Mkurugenzi Mkuu wa DW Peter Limbourg

### Mwandishi asimamishwa kazi kwa kumtaja mgonjwa wa UVIKO-19

Mnamo tarehe 20 mwezi Aprili 2020, Mwandishi Talib Ussi Hamad wa gazeti la *Tanzania Daima* alisimamishwa kazi kwa miezi sita kwa kumtaja mgonjwa wa Corona bila idhini yake. Anasema alishinikizwa kuomba msamaha, lakini akakataa kwa misingi kuwa taarifa aliyoitoa ilikuwa na manufaa kwa wananchi. Alidaiwa kukiuka maadili ya uandishi na alishtakiwa chini ya sheria Namba 5 ya Usajili wa Mawakala wa Habari, Magazeti na Vitabu ya mwaka 1988 na marekebisho yake Namba 8 ya mwaka 1997.

Hamad aliwasilisha kesi kwenye Mahakama Kuu ya Zanzibar mnamo mwezi Julai mwaka huohuo. Hatimaye, Serikali ya Zanzibar iliondoa amri hiyo ya kumsimamisha kazi Hamad mnamo mwezi Agosti mwaka 2020.

Lengo haswa la utoaji leseni ni kuhakikisha kuwa jukumu la kufahamisha umma linaachiwa watu wenye ujuzi wa taaluma ya uandishi habari na maadili mema. Lakini — kama ilivyodhihirishwa na kesi hii, na ile ya kufungiwa kwa muda magazeti ya *Mwananchi* na kituo cha Televisheni cha *Kwanza Online TV* — uwezo wa kutoa leseni kwa vyombo vya habari unaweza kutumiwa kama chomo cha kisiasa, kuwazuia wakosoaji wa serikali au waandishi wa kujitegemea kuweza kutekeleza majukumu yao. Kwa sababu hii, na kwa kuwa haki ya kila mtu kujieleza kupitia vyombo vya habari ni ya kila mtu, bila kujali maadili ya mhusika, utoaji leseni kwa wanaofanyakazi na vyombo vya habari, ni sawa na kuvunja haki ya uhuru wa kujieleza.

# Sheria inayosimamia upatikanaji wa taarifa na uhuru wa vyombo vya habari wakati wa UVIKO-19

## Sheria ya uhalifi wa kimitandao ya mwaka 2015

Lengo kuu la sheria hii ni kulinda miundombinu, kupunguza unyanyasaji wa kimitandao na kupunguza uharibifu umbao huenda ukatokea kwa njia hii.Hata hivyo, lengo hili limelaumiwa kote duniani kwa kukiuka haki za binadamu, ikiwemo na shirika la ARTICLE 19.

Maelezo ya sheria hii ni mapana mno kuweza kufafanuliwa kivingine na kwa hiyo inaweza kutumika vibaya kuwakandamiza wananchi. Sheria hii pia inafanya mtu yoyote kushtakiwa na kosa la jinai kwa kupatikana na taarifa ambazo hazijathibitishwa, na inaweza kutumiwa vibaya na vyombo vya usalama, ambao wana uwezo wa kumchunguza mtu yoyote anayepatikana na taarifa kama hizo bila idhini ya mahakama.

Ni kutokana na mapungufu kama haya, ndio polisi waliweza kutumia sheria hii kuwakamata na kuwafungulia mashtaka Haidary Hakam na Alona Tarimo kutoka gazeti la *Mwananchi* kwa kusambaza habari "zisizo za kweli" kuhusu UVIKO-19 kupitia mtandao wa WhatsApp.
.

## Sheria ya Takwimu 2015

Kifungu cha 37 (4) na (5) cha Sheria ya Takwimu ya mwaka 2015 kinaonyesha kwamba ni kosa la jinai kwa kituo chochote cha redio, televisheni, gazeti au jarida, ama tovuti au chombo chochote cha mawasiliano "kuchapisha" taarifa za takwimu ambazo "sio za kweli" au kwa "wakala au mtu yoyote" kuchapisha taarifa rasmi za takwimu lakini ambazo huenda zikapotosha ukweli.

Chini ya kifungu hiki cha taarifa rasmi za takwimu, huenda ikamaanisha kwamba uchapishaji wa takwimu za aina yoyote — bila kujali chanzo chake, ambacho huenda pia kikasemekana kuwa sio cha ukweli — ikachukuliwa kumaanisha kupotosha ukweli uliopo na kisheria inavutia faini ya sio chini ya shilingi milioni mbili za kitanzania (sawa na Dola 1200 za kimarekani) au kwenda jela kwa kifungo sio chini ya miezi sita au yote mawili.

Takwimu ni muhimu sana katika kueneza ufahamu wa UVIKO-19, jambo ambalo serikali ya Tanzania imejaribu kuzuia kwa njia zote tangu kuzuka kwa ugonjwa huu. Kwa sababu hiyo basi, hakuna habari muhimu zilizowafikia wananchi wa Tanzania, au dunia nzima kwa jumla kuhusu ugonjwa wa Corona kutoka humu nchini.

## Kanuni za Udhibiti Mawasiliano ya Posta na Kielektroniki (Habari za Mtandaoni) 2020

Sheria hii ambayo ilianza kutekelezwa mnamo tarehe 17 mwezi Julai 2020, imekuwa ikidhalilisha uhuru wa vyombo vya habari. Kwani sheria hii ilianzisha utoaji leseni na kutoza ushuru wanablogi, mazungumzo ya mitandaoni, na watumiaji wa tovuti na kukandamiza uhuru wa wanahabari wa mitandaoni, haki ya kutoingiliwa na mtu yoyote na upatikanaji wa habari.

Shirika la ARTICLE 19, lilikemea vikali kutekelezwa kwa sheria hizi na kutaka zitupiliwe mbali kwa ujumla wake. Sheria iliyokuwepo hapo awali (ile ya mwaka 2018) ilitumika kuwashtaki wana-habari na kufutilia mbali leseni za vyombo vya habari.

# Uhuru wa kujieleza kulingana na sheria za kimataifa

Uhuru wa kujieleza umedhaminiwa chini ya Azimio la Kimatiafa la Haki za Binadamu, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Raia na Haki za Kisiasa (ICCPR), Hati ya Haki za Binadamu na Watu wa Afrika, Tamko la Umoja wa Afrika kuhusu Uhuru wa kujieleza na upatikanaji wa habari barani Afrika na pia kwenye Katiba ya Tanzania.

Lakini wakati haki ni muhimu, sio thabiti. Chini ya sheria za kimataifa, uhuru wa kujieleza unaweza kuwa na mipaka kwa nia ya kukinga afya ya umma — lakini mipaka hiyo sharti iwe ya **halali**, **muhimu** na yenye **uwiano** (Makala ya 9 ya ICCPR).

# Mapendekezo

Shirika la ARTICLE 19 linatoa mapendekezo yafuatayo kwa serikali ya Tanzania:

- **Kutathmini sheria na vikwazo ilivyoweka kuzuia kusambaa kwa virusi vya Corona** na kuhakikisha kwamba sheria hizo zinaambatana na zile za kimataifa, kuhusu uhuru wa kujieleza na uhuru wa kupokea habari.

- **Kuchambua upya kwa sheria zilizopo kuhusu uhuru wa kujieleza,** ikiwemo uhuru wa vyombo vya habari, kuhakikisha kwamba zinalingana na Hati ya Haki za Binadamu na Watu wa Afrika pamoja na Tamko la Umoja wa Afrika kuhusu Uhuru wa kujieleza na upatikanaji wa habari barani Afrika na Azimio la Kimatiafa la Haki za Binadamu.

- **Kuondoa vifungu vyote vya sheria zinazosema ni uvunjaji wa sheria kwa "habari zisizo za kweli"** na kuhakikisha kwamba sheria na kanuni zote zinazohusu UVIKO-19 zinaambatana na viwango vya kimataifa kuhusu uhuru wa kujieleza.

- **Kufuatia mapendekezo yetu ya hapo awali, kufutilia mbali Kanuni za Udhibiti Mawasiliano ya Posta na Kielektroniki (Habari za Mtandaoni) ya mwaka 2020** na kuhakikisha kuwa kielelezo Kanuni za Udhibiti Mawasiliano ya Posta na Kielektroniki (Habari za Mtandaoni) 2021 hayatekelezwi**.**

- **Kutekeleza sera ambazo zitaboresha utendakazi wa wana-habari na kutambua mchango wao muhimu katika kuangazia haki za binadamu,** ikiwemo kuhakikisha kwamba kutiwa mbaroni kiholela kwa wana-habari, kushtakiwa kwa kufanya kazi zao, hakutavumiliwa kamwe na kuhakikisha wale wanaohusika wamechukuliwa hatua za kisheria.

- **Kuchunguza ripoti zote za ukiukaji wa haki za binadamu dhidi ya wana-habari** na kuhakikisha kwamba wote waliotekeleza vitendo hivyo—ikiwemo maofisa wa usalama—wamechukuliwa hatua za kisheria kulingana na viwango vya kimataifa.

- **Kutekeleza mapendekezo ya azimio kuhusu usalama wa wana-habari,** lililotekelezwa na Baraza la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Binadamu mnamo tarehe 6 Oktoba 2020, azimio ambalo linatoa mwelekeo kuhusu usalama wa waandishi haswa wakati huu wa kuwepo kwa janaga la UVIKO-19.

.

Ushahidi uliwasilishwa kwenye ripoti hii ulitolewa kutoka kwenye vyombo vya habari ,mashirika yanayotetea haki za wana-habari, vyama vya waandishi habari na tathmini za kisheria kati ya mwezi Machi 2020 na Julai mwaka 2021.Ushahidi huu unaangazia zaidi ukiukaji wa haki za waandishi wa habari kwa kutilia maanani msimu huu wa UVIKO-19 ( na wala sio ukiukaji wa haki za binadamu unaohusiana na visa vyengine visivyohusu waandishi wa habari). Kwa maelezo zaidi tembelea: www.article19.org/covid-19-response-in-africa